

**HOTUBA YA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KWENYE SIKU YA
SHERIA NCHINI, TAREHE 01 FEBRUARI, 2024**

- *Mheshimiwa Prof. Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania,*
- *Mheshimiwa Khamis Ramadhan Abdalla, Jaji Mkuu wa Zanzibar,*
- *Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani,*
- *Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb) Waziri wa Katiba na Sheria,*
- *Mheshimiwa Augustine Mwarija (Dean wa Majaji wa Mahakama ya Rufani) na Waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Rufani wengine mliopo,*
- *Mheshimiwa Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania,*
- *Mheshimiwa Jaji Imani Aboud, Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu,*

- *Mheshimiwa Jaji Nestor Kayobera, Rais wa Mahakama ya Afrika Mashariki,*
- *Waheshimiwa Majaji wa Mahakama Kuu, wa Tanzania Bara na Zanzibar mliopo,*
- *Waheshimiwa Majaji Wakuu wastaafu na Majaji Wastaafu,*
- *Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali,*
- *Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, Katibu Mkuu wa CCM, Uongozi wa Mkoa Pamoja na Vyama vingine vya Siasa;*
- *Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote mliopo,*
- *Mhe. Balozi Dkt. Moses Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi,*
- *Bi. Mary Makondo, Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, na Makatibu, Wakuu wengine na Naibu Makatibu Wakuu Mliopo,*
- *Bi. Nenelwa Mwihambi, Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,*

- *Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania,*
- *Bw. Mbarouk Khai, Mtendaji Mkuu wa Mahakama Zanzibar na watumishi wote kutoka Mahakama ya Zanzibar mliopo nasi,*
- *Mheshimiwa Sylvester Joseph Kainda, Kaimu Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania,*
- *Mheshimiwa Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma na Wakuu wa Wilaya Mliopo,*
- *Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama,*
- *Ndugu Harold Sungusia, Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika,*
- *Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa mliopo,*
- *Wasajili, Wakurugenzi na Watendaji wa Mahakama mliopo,*
- *Mahakimu na Mawakili na watumishi wote wa Mahakama,*
- *Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma,*

- *Viongozi wa Dini mliopo,*
- *Ndugu Wanahabari, Wageni waalikwa, wanafunzi, Mabibi na Mabwana.*

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...!

UTANGULIZI

Ndugu zangu,

Naomba nami mniruhusu niongeze sauti yangu, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai iliyotuwezesha kukutana hapa leo katika Siku hii adhimu, siku ya Sheria inayoashiria kuanza kwa shughuli za Mahakama kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Jaji Mkuu,

Moja kati ya sifa inayonasibishwa na kada ya wanasheria ni namna mnavyojifautisha na kada nyingine. Mbali na mavazi mnayovaa, lugha mnayotumia na zile mbwembwe za kilatini na mengine; lakini pia umakini na madaha mkiwa kazini. Akisimama Mwanasherri/Wakili,

unajua pale kazi ipo. Lakini pia mnajitofautisha kwa namna mnavyouanza mwaka, kwa kuadhimisha siku hii adhumu ya Sheria.

Kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kukutana na kundi lenu ndani ya mwaka huu, niwatakie kheri ya miaka mipyä miwili; mmoja, mwaka mpyä wa kalenda wa 2024 lakini wa pili, mwaka mpyä wa Mahakama. ***Heri ya Mwaka mpyä!***

Nitumie fursa hii kukushukuru sana Mheshimiwa Jaji Mkuu kwa mara nyingine tena kunikaribisha kuwa Mgeni Rasmi kwenye shughuli hii adhimu. **Ahsante sana!**

Katika siku hii, ninawiwa kuwapongeza Waheshimiwa Mahakimu, Wasajili, Majaji wa Mahakama Kuu, Majaji wa Mahakama za Rufani na watumishi wote wa Mahakama kwa namna mnavyoendelea kutekeleza majukumu yenu. Ongezeko la imani ya wadau kwenu kutoka **65%** mwaka 2015 mpaka **78%** mwaka 2019 na **88%** mwaka 2023 kama ilivyooneshwa kwenye Ripoti ya REPOA ni ushahidi tosha kwamba mnafanya kazi kubwa na kwamba Mahakama inakwenda na mabadiliko, na ndio maana imani ya watumiaji wa Mahakama nayo inaongezeka. Hata hivyo, **Mheshimiwa Jaji Mkuu**, lile angalizo la REPOA, nami nasisitiza liangaliwe kwa karibu zaidi.

Kama kawaida yenu katika kipindi cha Wiki ya Sheria kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali za Serikali, mmetoa masaada wa kisheria na huduma zenu kwa umma na kueleza kwa umma kuelezea hatua mbalimbali zinazochukuliwa katika kuimarisha huduma za Mahakama nchini. Ilikuwa ni Wiki yenyе manufaa kwa wananchi waliohitaji msaada wa kisheria. *Hongereni sana!*

Nawapongeza pia Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS). Nimeona maoni, mapendekezo na maombi yaliyopevuka. *Maturity* (ukomavu) inaonekana ndani ya TLS. Nilikuwa namsikiliza vizuri Sungusia, alivyotulia na kumimina maneno ya hekima, na ameomba kwa ustaarabu mkubwa sana. Kwa hiyo nawapongezeni sana, na yote tumeyasikia.

Katika hatua nyingine, nishukuru sana wageni wetu, wakufunzi wa masuala ya *Financial Crimes* kutoka UK na Ireland walioko hapa, tunawaambia karibuni sana. *Thank you very much!*

Sitosita pia kuwapongeza wanakwaya, kweli ni kwaya ya kimahakama, Nawapongezeni kwa ujumbe mzuri na muafaka kwa siku ya leo. Nilikuwa nanong'ona na Mheshimiwa Spika, nikamwambia, ninataka kuanzisha ligi ambayo nitaidhamini mwenyewe, ligi ya mihimili mitatu: kwaya ya Utumishi Serikalini, kwaya ya Mahakama na Kwaya ya

Bunge. Tuone nani zaidi. Sasa wenyewe mtajipanga, lakini mimi nitadhamini hiyo ligi.

Mheshimiwa Jaji Mkuu,

Nakushukuru kwa uongozi wako mahiri unaoleta mabadiliko chanya katika utoaji wa huduma za Mahakama na kuendana na dhamira ya Serikali ya kuendelea kuimarisha mifumo ya utoaji haki nchini. Hivyo, mafanikio uliyoyabainisha kwenye hotuba yako yanaonesha mwelekeo mzuri na kwa kweli yanatupa faraja. ***Hongereni sana***

Kauli Mbiu na Ripoti ya Tume ya Haki Jinai

Mheshimiwa Jaji Mkuu

Kauli mbiu ya maadhisho ya mwaka huu inasema “***Umuhimu wa Dhana ya Haki kwa Ustawi wa Taifa: Nafasi ya Mahakama na Wadau katika kuboresha Mfumo Jumuishi wa Haki Jinai***”. Hapa nafarijika kwamba, Mahakama imejidhatiti kutimiza wajibu wake katika maboresho ya Mfumo Jumuishi wa wa Haki Jinai, kama ilivyoelezwa kwenye Hotuba ya Jaji Mkuu. Mwelekeo huu ni mwendelezo wa utekelezaji wa Mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai unaofanywa na Mahakama na Taasisi nyingine za Haki Jinai. Serikali kwa upande wetu, tunaendelea na

Makakati wa namna ya kutekeleza Mapendekezo mengine ya kisera na kisheria.

Juhudi za Serikali kuimarisha utendaji wa Mahakama

Mheshimiwa Jaji Mkuu,

Ibara ya **120** ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) (2020-2025) inaitaka Serikali pamoja na mambo mengine, *kuchukua hatua zaidi za kupunguza mrundikano wa kesi mahakamani; kuimarisha vyombo vya sheria kwa kuongeza wigo wa huduma za utoaji wa haki nchini; na kujenga mifumo ya TEHAMA na kuendelea kuhimiza matumizi yake katika utoaji wa haki.*

Katika kutekeleza maelekezo hayo ya Ilani ya Uchaguzi, Serikali imeendelea kushirikiana na Mahakama kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili Mahakama kwa lengo la kuongeza ufanisi na mambo yote yamesemwa hapa na Mheshimiwa Jaji Mkuu. Lakini vilevile, Mheshimiwa Mwakasheria Mkuu wa Serikali naye ameeleza ya upande wao.

Pamoja na uwekezaji mkubwa kwenye TEHAMA kama ulivyoiezwa vizuri, Serikali pia imeendelea kuimarisha utendaji wa Mahakama kwa ujenzi wa majengo ya kisasa ya Mahakama maarufu

kama Vituo Jumuishi vya kutolea haki; na kuongeza idadi ya watenda kazi kila hali ya uchumi inaporuhusu. Kwa mfano, idadi ya majaji wa Mahakama ya Rufani imeongezeka kutoka majaji **16** mwaka 2021 hadi majaji **35** mwaka 2023, hili ni ongezeko la **118%**. Aidha, idadi ya majaji wa Mahakama Kuu imeongezeka kutoka **63** mwaka 2021 hadi **105** mwaka 2023, ongezeko la **67%**. Vilevile idadi ya Mahakimu Wakazi imeongezeka kutoka **1,098** mwaka 2021 hadi Mahakimu **1,146** mwaka 2023.

Ni matazamio yetu kwamba uwekezaji mkubwa uliofanywa kwenye ujenzi wa majengo, utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA na ongezeko la idadi ya majaji na watenda kazi utajidhihirisha kwa kuongeza ufanisi zaidi na wananchi wataona utofauti huo. Uzuri ni kwamba, hata Ripoti ya REPOA imeona utofauti huo, na wameona kuridhishwa kwa wananchi na huduma za Mahakama. Kwa hiyo na hapa napo nataka niwapongeze.

Hotuba ya Jaji Mkuu

Mheshimiwa Jaji Mkuu,

Hotuba yako ilikuwa na masuala mahususi na yale ya ujumla. Kwenye masuala mahususi, pamoja na mambo mengine, ulibainisha hatua kubwa zilizopigwa katika matumizi ya TEHAMA. Umetoa mapendeleko kuhusu hatua za kuchukua katika kuunganisha mifumo ya

TEHAMA mionganini mwa Taasisi za Haki Jinai. Vilevile umependekeza iundwe Timu ya Pamoja ya wadau wote wa haki jinai ili kuangalia njia bora ya kuunganisha mifumo yao ya TEHAMA.

Huu ni ushauri mzuri. Hatua hii sio tu itapunguza hali ya mifumo kutosomana, bali pia itaongeza ufanisi wa kazi baina ya taasisi zote husika. Hivyo, tumelipokea na hapa namuona Waziri wangu Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora na Katibu Mkuu wako hapa. Naomba kupitia eGA mzidishe ushirikiano na Wizara ya Katiba na Sheria, Waziri yuko hapa. Muendelee kuratibu utekelezaji wa pendekero hili, haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Jaji Mkuu,

Umezungumzia pia suala la maslahi ya watumishi wa TEHAMA katika Mahakama. Nakubaliana na maoni yako kwamba, watumishi hao waangaliwe vizuri, kwa sababu wamekuwa sasa ni nyara ya Mahakama, *wanawindwa!* Kwa hiyo, muwaangalie vizuri. Ni imani yangu kuwa hili liko ndani ya uwezo wa Mtendaji wa Mahakama.

Ni vizuri kubuni mbinu mbalimbali za kutoa motisha kwa watumishi hawa na wengine wanaofanya kazi zao kwa ubunifu, uadilifu na weledi wanaowezesha taasisi kuongeza ufanisi. Sasa msipowatunza,

wengine wanaowatolea macho watakuja kuwachukua na kuwapa madonge manono na nyie muanze upya. Na mkianza upya mtarudi nyuma.

Mheshimiwa Jaji Mkuu,

Nikigusia masuala uliyoyaita ya jumla, ulizungumzia mfumo wa haki jumuishi kwenye masuala mbalimbali kama yalivyoainishwa kwenye Ripoti ya Tume ya Haki Jinai. Baadhi ya masuala hayo ni kuongeza bajeti ya vikao vyta Mahakama (*high court sessions*), matumizi ya adhabu mbadala na hitajio la kutunga sheria ya dhamana. Serikali tayari tumeunda Timu ndogo inayotuandalia Mpangokazi wa utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai, kama mlivyomsikia Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Lakini pia Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lile ombi lako la vituo jumuishi vyta sheria, sasa lionekane kwenye Mpangokazi huo, ili ikatekelezwe pamoja na yale mtakayoleta kwenye Mpangokazi wa kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai. Bila shaka yote yaliyoainishwa, yatazingatiwa kikamilifu.

Mama Samia Legal Aid Campaign

Mheshimiwa Jaji Mkuu,

Hotuba yako pia imegusia juhudini za kuimarisha upatikanaji wa huduma za kisheria kwa wananchi wasio na uwezo kupitia **Mama Samia Legal Aid Campaign**. Mazingira ya jamii yetu, yalitulazimu kuanzisha Programu hiyo. Kama alivyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali, malalamiko ni mengi. Kila pembe kuna malalamiko, tukaona kama Serikali kuna umuhimu wa kuanza na Kampeni hii.

Tunashukuru kwamba, Kampeni hii imepokelewa vizuri na wananchi. Na niseme Kampeni hiyo inaendelea vizuri, na kwa jinsi ilivyopokelewa, ni wazi kuwa, kuna uhitaji mkubwa wa msaada wa kisheria hapa nchini. Tayari Kampeni hiyo imewafikia wananchi **383,293** katika Mikoa 6 ya Dodoma, Manyara, Shinyanga, Ruvuma, Simiyu na Singida. Kupitia Kampeni hiyo, migogoro **takriban 511** ilitatuliwa. Aidha, Kampeni imetusaidia kubaini maeneo yepi yana migogoro mingi zaidi kwenye jamii zetu, na tumbaini kwamba, maeneo ya ardhi, matunzo ya watoto, ndoa, mirathi, ukatili wa kijinsia na madai; ndio maeneo yenye malalamiko makubwa sana.

Sasa niitake Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na wadau kutekeleza kikamilifu mfumo wa utoaji wa msaada ya kisheria kwa

mujibu wa Sheria. Hili ni jambo jema, na kama wasemavyo wadau wa msaada wa sheria, *legal aid is not an expense, but an investment in social justice.* Kwa tafsiri isiyo rasmi, ni kwamba, msaada wa kisheria sio gharama, lakini ni uwekezaji kwenye haki za watu. Hivyo, wale wote wanaoguswa na haki za jamii, tunaomba wajitokeze na kuunga mkono jitihada hizi. Hapa tunawekeza kupatikana kwa haki za watu.

Jambo jingine uliloligusia Mheshimiwa Jaji Mkuu, ni ushirikiano katika kujitathmini na kubaini mapungufu yetu katika Taasisi zetu, nami nakuunga mkono kwenye hilo. Kama ulivyofanya kwa REPOA, niombe Taasisi nyingine zote, tushirikiane kwenye kujitathmini, kubaini mapungufu na tuchukue hatua kwa pamoja kurekebisha mapungufu tutakayoyabaini.

Kuimaraisha Haki Madai

Mheshimiwa Jaji Mkuu,

Kama nilivyokwisha elezea, jitihada kubwa zimefanyika kwa lengo la kuimaraisha mfumo wa Haki Jinai. Na kwa kuwa tunaendelea na mchakato wa kuimaraisha mfumo wa Haki Jinai hapa nchini, kwa kuwa

hatua za Haki Jinai zinaendelea, tunasubiria Mpangokazi ili tuutekeleze, kuelekea kwenye upatikanaji vyema na mtiririko wa kupatikana haki.

Nimeona nichokoze pia kuangalia vilevile, umuhimu wa kuimarisha mfumo wa Haki Madai. Na kwenyewe pia kuna malalamiko. Kesi zinacheleweshwa, mzunguko ni mkubwa. Kwa mfano katika Mahakama za Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Hakimu Mkazi inachukua hadi miezi 12 kwa shauri kusikilizwa hadi kuhitimishwa. Kwa upande wa Mahakama Kuu, sijui baada ya marekebisho haya kuchukuliwa, lakini inachukua hadi miezi 24 kwa shauri kusikilizwa hadi kutolewa hukumu. Sasa hii inachukua muda mwingi wa wadau wanaohusika kwenye mashauri haya, na wanapoteza muda wa kufanya mambo mengine muhimu kwa jamii. Kwa hiyo niombe sana na huko nako kutupiwe jicho , kufanyiwe maboresho na haki kwa upande wa madai iweze kupatikana.

Jambo jingine ambalo kwa mara nyingine nataka kulitilia mkazo, ni kuharakishwa kusililizwa kwa kesi za kibiashara. Tunapovutia mitaji na uwekezaji katika nchi yetu, na kufungua fursa za kibiashara, tunatambua kwamba uwekezaji huambatana na masuala ya kisheria na migogoro ya kibiashara. Ni vyema kwa Mahakama zetu kutoa umuhimu kwa mashauri ya aina hiyo pia.

Mheshimiwa Jaji Mkuu,

Ibara ya **107A(2)(a)-(e)** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka Kanuni za kuzingatiwa pindi Mahakama zinapotoa uamuzi wa Mashauri mbalimbali. Kanuni hizo ni *kutenda haki kwa wote bila ya kujali hali ya mtu kijamii na kiuchumi; kutochelewesha haki bila sababu ya msingi; kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro na kutenda haki bila kufungwa kupita kiasi na masharti ya kiufundi yanayoweza kukwamisha haki kutendeka.*

Hapa Mheshimiwa Jaji Mkuu, nataka nikupongeze tena, wewe na Mahakama. Hatua nyingi mlizochukua zimekwenda kupunguza mambo mengi kati ya haya tuliyoyasema. Ucheleweshaji wa kesi umepungua kwa kiasi fulani, lakini pia mmeanza kuchukua hatua za usuluhishi, kupunguza muda wa kesi kusikilizwa kwa muda mrefu Mahakamani. Lakini pia unapochukua hatua za usuluhishi unaharakisha kupatikana kwa haki, na haileti machungu na maovu.

Unajua hukumu inaleta uchungu na maumivu kwa anayehukumiwa, kwa yule ambaye haki haiendi upande wake, lakini usuluhishi wote wanakubaliana. Kwa hiyo inaondosha machungu na maovu. Kwa hiyo, ningeomba sana tuifuate Ibara ya **(107A(2)(a)-(e))** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) ambayo nimeisoma.

Ambayo ina mambo manne, moja ikiwa ni *kutenda haki kwa wote, kutochelewesha haki, kutofungwa kupita kiasi na masharti ya kiufundi na kutoa kipaumbele katika usuluhihi*.

Hivyo, Mheshimiwa Jaji Mkuu, Majaji, Mahakimu na Mawakili wa Serikali, tukitekeleza Ibara hiyo kwa dhati, maana yake tunajiepusha na kuahirisha mashauri mara kwa mara na hatutatumia muda mrefu wa Mahakama kushughulikia masharti ya kiufundi na kuwekeana mapingamizi yasiyoisha. Kwa sababu tukienda kwenye Mahakama huko, wenzetu ni mafundi sana kwa kutumia vipengele vyta Sheria, Mapingamizi mengi. Na kila Mapingamizi yakiwekwa, Jaji inabiadi aahirishe, aende kwanza akaangalie, pingamizi linasemaje, apange tena tarehe. Kwa hiyo tukienda kwenye usuluhihi, haya yote yanaondoka, na mambo yanakwenda kwa haraka zaidi.

Falsafa ya R4 na Haki Madai

Mheshimiwa Jaji Mkuu,

Upo uhusiano mkubwa kati ya haki na maendeleo ya kiuchumi. Tunapoendelea kuvutia mitaji nichini na kuongeza fursa za uwekezaji, ni lazima tuishi na kuzungumza lugha ya kibashara na uwekezaji. Mwekezaji anathamini sana muda, kwani muda ni mali. Na hapa

namaanisha mwekezaji wa ndani na yule wa nje, na ndio maana ni lazima mitazamo ya wadau wa Mahakama nchini ijielekeze kwenye kupunguza muda unaotumika kwenye mashauri ili wananchi watumie muda wao mwingi kwenye uzalishaji mali.

Lakini nataka pia nikupongeze kwa hatua mlizochukua, za sasa kufundisha Mahakimu wetu na Majaji masuala ya *Finacial Crimes* (makosa yanayohusisha fedha), kama mlivyofanya ndani ya Wiki hii, na wataalamu wetu wako hapa. Lakini nakumbuka kule nyuma, mliwahi kukaa na kuangalia mtatizama vipi masuala ya uwekezaji. Sasa haya yasiwe yanafanywa mara moja na kupita, bali yawe yanafanywa muda baada ya muda.

Nashauri Mahakama ziwe mstari wa mbele katika ***kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro*** na endapo wanaohusika wakilazimika kuendelea kupata haki Makakamani badala ya usuluhishi, basi Mahakama zisaidie mashauri yaishe mapema bila kuathiri ubora wa hukumu zinazotolewa. Mtakubaliana nami kwamba, **usuluhishi tofauti na Mahakama, hauachi makovu ya hasira** hivyo, kutoa nafasi kwa mahasimu kuendelea kufanya kazi pamoja licha ya kutofautiana.

Kwa hiyo ndugu zangu, usuluhishi unaweza kuwa na njia nyingine ya kuimarisha Haki Madai. Nitoe rai kwa Vitivo vya Sheria nchini, pamoja na Shule ya Sheria kuongeza kasi ya kuandaa wataalam katika tasnia ya usuluhishi nchini. Aidha, niitake Wizara ya Katiba na Sheria, kukaa na wadau wa Usuluhishi na kubainisha maeneo yanayotakiwa kufanyiwa kazi zaidi ikiwemo uwezekano wa hitajio la kutunga Sera ya Usuluhishi. Kwa upande mwingine Mawakili nao waanze kuiona fursa hii na kutafuta namna ya kunufaika nayo. Nchi nyingi zinazovutia mitaji na uwekezaji, mwelekeo wake ni utatuzi wa migogoro kwa njia za usuluhishi. Ni wakati muafaka nasi kama Taifa la Tanzania, tujielekeze huko.

Mahakama na Haki

Mheshimiwa Jaji Mkuu, na Ndugu zangu

Mnafahamu kwamba, kwa mujibu wa Ibara ya 107A-(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mamlaka yenyeye kauli ya mwisho ya utoaji haki nchini ni Mahakama zetu**. Hivyo, Mahakama ina dhima kubwa katika kutekeleza jukumu hili. Waheshimiwa Majaji na Mahakimu katika utendaji kazi wenu, mnapaswa kukumbuka kwamba kazi ya kutoa

haki, ni kazi ya Mungu, hivyo, mnawajibika kuifanya kwa uadilifu mkubwa.

Mimi naamini ukitoa hukumu ya dhulma, unajua kabisa kwenye nafsi yako kwamba umedhulumu haki ya mtu, au haki ya jamii. Alisema mmoja wetu hapa kwamba, Maandiko Matakatifu yanatuambia kwamba, dhambi ni aibu kwa jamii. Ukitoa hukumu ya dhulma, umetenda dhambi, na unaipelekea jamii aibu. Kwa nini aibu? Kwa sababu inawezekana kabisa uliyemdhulumu kwenda jela bila hatia ameacha familia, watoto na ndugu wategemezi. Wakikosa wa kuwahudumia ni aibu kwao, wanaadhirika, wanahangaika. Kwa hiyo, umefanya aibu kwa jamii. Sasa niwaombe sana kuzikanya nafsi zijiipushe kutoa hukumu za dhulma.

Mafundisho ya Kikristo na yale ya Kiislam yanafundisha kuhusu umuhimu wa haki. Biblia katika Mithali Sura ya 14, Mstari wa 34 na ametaja mmoja wetu hapa, inasema "*Haki huinua Taifa.*" Kwa upande wa dini ya Kiislam, tunaambiwa, *kwenye haki usisimamishe batili na kwenye batili haki haisimami*. Kwamba kwenye haki iwe haki na kwenye batili iwe batili; tusivichanganye. Unapochukua nafasi ya haki ukasimamisha batili basi umeshafanya dhambi na ile aibu ya jamii itakuandama.

Ndugu zangu, Majaji na Mahakimu, ninyi nyote mliapa mkiwa mmeshika vitabu vya dini zenu. Hivyo mnalazimika kusimama katika misingi ya haki, kama miongozo ya dini zenu inavyotaka. Pamoja na imani zenu za dini, lakini pia Katiba ambayo ndiyo Sheria mama, katika Ibara 107A imeweka Kanuni za kuzingatiwa. Moja ya Kanuni hizo ni *kutenda haki kwa wote bila ya kujali hali ya mtu kijamii na kiuchumi*. Hivyo, mna dhima kote kote, mna dhima mbinguni ya kutenda haki, kama mnavyotakiwa na Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, neno la kuondoka nalo kwenye kilele cha Wiki hii ya Sheria, ni *kutenda kwa haki*.

HITIMISHO

Mheshimiwa Jaji Mkuu;

Nirejee kutambua na kupongeza hatua kubwa za kimageuzi zilizofanyika kwenye muhimili wa Mahakama. Serikali inaendelea na itaendelae kuchukua hatua mbalimbali katika kuimarisha utendaji wa Mahakama nchini. Ulisema penye utashi wa kisiasa, basi lolote linawezekana, nami nataka nikuhakikishie, kama Mkuu wa Nchi, kwamba bado nasimama na kutaka haki ya watu isimame. Kwa hiyo takwa la kisiasa lipo, na tutajitahidi kutafuta rasilimali, za kukuwezesheni muweze kusimisha haki vema. Serikali itaendelea kusisitiza umuhimu wa Mahakama kutofungwa na masharti ya kiufundi, na kuhimiza matumizi ya usuluhishi. Nirejee pia rai yangu kwa Mahakimu na Majaji kusimama daima katika misingi ya haki.

Nihitimishe hotuba yangu kwa kumshukuru tena Mheshimiwa Jaji Mkuu kwa kunialika kwenye shughuli hii iliyofana. Niwashukuru pia wananchi wote mliohudhuria na mnaofuatilia kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Ni matumaini yangu, hotuba hii itakuwa na mchango katika utendaji kazi wa wadau wote wa Mahakama nchini tunapouanza rasmi mwaka wa Mahakama na itawakumbusha kufanya kazi kwa kuzingatia viapo vyenu. Ninaposema wadau wa Mahakama, ni pamoja na wengine, mnaofanya kazi nao, Mwanasheria Mkuu, DPP (Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali), Polisi na wote, waliotajwa na wanakwaya kama ni wadau, basi haya mwende mkayazingatie.

Baada ya kusema haya, Mheshimiwa Jaji Mkuu, Waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Rufani, Waheshimiwa Majaji wa Mahakama Kuu, Waheshimiwa Wasajili, Mahakimu na Watendaji wote wa Mahakama. Sasa natamka rasmi kwamba, **MWAKA MPYA WA MAHAKAMA, SASA UMEZINDULIWA RASMI.**

Nimuombe Mungu Aibariki nchi yetu Tanzania

Ahsanteni sana